

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKARI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA**

Shule ya Sekondari Chihangu,

S.L.P 79,

Newala.

Tarehe .....

Kumbukumbu Na CHSS/G1/01/10

MWANAFUNZI .....

.....

S.L.P .....

**YAH : MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHIHANGU WILAYANI  
NEWALA, MKOA WA MTWARA MWAKA 2021**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2021** hongera sana. Shule ya Sekondari Chihangu ipo umbali wa km 5 kusini/magharibi mwa nji mkuu wa wilaya ya newala Kitangari. Shule hii ipo katika kata ya chihangu ni shule ya kutwa. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **04/01/2021**

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE**

**A. WAVULANA**

- i. Suruali rangi ya damu ya mzee mshono wa kawaida siyo modo isiyozidi mifuko mitatu chini upana 7, pea mbili (2)
- ii. Mashati mwawili tetroni mikono mifupi meupe(2)
- iii. Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili (2)
- iv. Soksi nyeupe jozi mbili (2)
- v. Sweta rangi ya damu ya mzee

**B. WASICHANA**

- i. Sketi ya rinda 3 pembeni, ndefu inayofunika viatu jozi (2) rangi damu yam zee
- ii. Mashati mwawili tetroni mikono mifupi meupe(2)
- iii. Viatu ya ngozi rangi nyeusi jozi mbili (2)
- iv. Soksi nyeupe jozi mbili (2)
- v. Hijabu nyeupe (si lazima)

## **2.2 NGUO ZA KAZI**

### **A. WAVULANA**

- i. Suruali mbili rangi nyeusi zisizo modo
- ii. Fulana moja rangi ya bluu

### **B. WASICHANA**

- i. Gauni rangi ya bluu mbili (2)
- ii. Hijabu ya bluu (si lazima)

## **3.0 SARE YA MICHEZO**

### **A. WAVULANA**

- i. Track suruali rangi ya bluu.
- ii. Jezi ya Tanzania rangi ya bluu.
- iii. Raba jozi moja.
- iv. Soksi nzito rangi yoyote.

### **B. WAVULANA**

- i. Track suruali rangi ya bluu.
- ii. Jezi ya Tanzania rangi ya bluu.
- iii. Raba jozi moja.
- iv. Soksi nzito rangi yoyote

## **4.0 VIFAA VYA DARASANI**

- i. MKEBE (MATHEMATICS SET 1)
- ii. DAFTARI KUBWA TISA (COUNTER BOOK)
- iii. DAFTALI NDOGO TISA KWA AJILI YA MAZOEZI
- iv. PENI
- v. KALAMU
- vi. KIFUTIO
- vii. RULA
- viii. KAMUSI YA KIINGEREZA, BASIC ENGLISH, OXFORD
- ix. REAM PAPER MOJA (Inakabidhiwa siku ya kuripoti shuleni)
- x. BIMA YA FYA ( Fedha taslimu Tsh. 5000)

## **5.0 VIFAA VYA KAZI ZA MIKONO**

- i. Jembe katika mpini wake (ngwamba)
- ii. Fyekeo/panga 1  
(vitakaa shuleni)

## **6.0 CHAKULA CHA WANAFUNZI**

- i. Mahindi kg 40
- ii. Maharage au njugu kg 20

iii. Mpishi na kusaga Tsh. 20,000/=

## **7.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na 10 ya mwaka inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Raisi TAMISEMI yenye jukumu mla usimamizi na uendeshaji Elimu.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, walimu, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la msingi.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote.
- e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

## **8.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHWA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

- a. Wizi
- b. Uasherati na ushoga
- c. Ubakaji
- d. Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli. n.k
- e. Kupigana au kupiga mtu
- f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g. Kudharau bendera ya taifa na wimbo wa taifa
- h. Kuoia au kuolewa
- i. Kutoa mimba
- j. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki katika kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- k. Kukataa adhabu kwa makusudi
- l. Kuwa na simu ya mkononi

## 9.0 FOMU YA MAKUBALIANO NA MZAZI/ MLEZI

Mimi ..... ambaye mzazi/ mlezi wa ..... nakubali masharti yafuatayo :-

- a. Nafasi aliyopewa kijana wangu kujiunga na kidato cha kwanza katika mwaka wa masomo .....
- b. Kijana wangu kufuata sheria, magizo na masharti yote ya shule ya sekondari Chihangu
- c. Kulipa michango yote itakayoelekezwa na shule hususani “michango ya chakula”
- d. Kumpatia mwanangu mahitaji yote ya shule
- e. Kufatilia kwa karibu maendeleo ya mwanangu kitabia na kitaaluma
- f. Kupokea taarifa zote kutoka shuleni zinazomhusu mwanangu na kuzifanyia kazi kwa wakati

Ahsante

JINA ..... SAHIHI ..... TAREHE .....

## 10.0 VIAMBATANISHO

- a. Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa na mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b. Kivuli cha cheti cha kuzaliwa
- c. Fomu ya mzazi/ mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
- d. Mkataba wa kutoshiriki migomo, vurugu, ama makosa ya jinai
- e. Taaifa binafsi kuhusu mwanafunzi

Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

Karibu sana katika shule hii

.....  
KHADIJA N. YAHAYA

MKUU WA SHULE

0656577086

NB:

- Tafadhali lete kivuli cha cheti cha uzaliwa (photocopy) na siyo kiapo kutoka mahakamani
- Kama hujaelewa tafadhali fika shuleni upate maelekezo sahihi
- Kamwe usikubali maelekezo ambayo si ya shule

**NEWALA DISTRICT COUNCIL**  
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION-STUDENTS**

**PART ‘A’**

FROM;  
HEADMISTRESS,  
CHIHANGU SECONDARY SCHOOL,  
P.O.BOX 79,  
**NEWALA.**

TO : MEDICAL OFFICER I/C

.....  
.....  
.....

Please Examine ..... Age .....

- As to his/her fitness to continual with Secondary Education.

**PART ‘B’**

(To be completed by a Medical officer )

Please examine the following and comment

- a. Eye sight.....
- b. Hearing.....
- c. Speech.....
- d. Syphilis test.....
- e. Blood pressure.....
- f. Pregnancy (for girls only).....
- g. Ulcers.....
- h. Any other physical disability.....

**PART ‘C’**

(To be completed by Medical Officer)

- I have examined the above named student and I recommended that he/she is physical fit/unfit for admission in Secondary Education

Date.....

Signature.....

Station.....

Designation.....

- Delete as appropriate  
Delete whichever not applicable